



TAARIFA KWA UMMA

NJIA MPYA ZA USAJILI WA LESENI MKOANI DAR ES SALAAM

*Dar es Salaam,
24 Januari, 2024.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawakaribisha wasafirishaji kuomba leseni kwenye njia mpya za daladala Jijini Dar es Salaam, ili kufikisha huduma karibu na wananchi kwa mabasi yanayokidhi vigezo kama ifuatavyo;

N A	KUTOKA	KWENDA	KUPITIA BARABARA YA	UJAZO WA BASI KUANZIA ABIRIA	IDADI
1	MWENGE	MBAGALA RANGI TATU	SAMNUJOMA, MANDELA, KILWA	26	20
2	MWENGE	MBAGALA RANGI TATU	BAGAMOYO, KAWAWA, KILWA	26	20
3	KIGAMBONI	VIJIBWENI HOSPITAL	KISIWANI	15	20

KUONGEZA IDADI YA MAGARI KATIKA NJIA IFUATAYO

1.	KIGAMBONI	CHEKA	MJIMWEMA	25	20
----	------------------	--------------	-----------------	-----------	-----------

Vigezo vya kuzingatia:

- Magari yenye usajili kuanzia namba **DXA** kwa njia za kuanzia/kuishia stendi mpya ya **Mwenge**
- Kwa gari jipya ambalo halijawahi kusajiliwa katika mfumo wa utoaji leseni wa RRIMS, dereva wa gari husika atapaswa kuthibitishwa LATRA
- Sare kwa magari ya njia za Mwenge; Dereva na Kondakta wanatakiwa kuvali suruali yenye rangi **Nyeusi** na shati la mikono mifupi lenye rangi ya **Bluu bahari** (Sampuli ya sare inapatikana kwenye ofisi ya LATRA Mkoa wa Dar es Salaam)

**Imetolewa na:
Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**